FUNZO LA 6

1. Mwanzo ni lini?
-Mwanzo ni kitambo sana, wakati Mungu alipoumba vitu vyote.

2. Hapo mwanzo, nani aliyeumba vitu vyote vilivyomo ulimwenguni?
-Mungu.

3. Ni nini kilichokuwa ulimwenguni kabla ya Mungu kuumba vitu vyote?
-Hakuna.

4. Kama hakukuwa na chochote, basi Mungu alitumia nini kuumba vitu vyote?
-Hakuna.

5. Kwa hivyo Mungu aliumba vipi ulimwengu?
-Mungu aliumba ulimwengu bila chochote.

6. Mungu aliwezaje kuumba kila kitu kutoka kwa kisichokuwepo?
-Mungu ni mwenye nguvu zote.
-Nguvu za Mungu haziishi.
-Nguvu za Mungu ni za milele.

7. Je, kuna kipimo kwa nguvu za Mungu?
-La.



8. Je, Shetani, mapepo au watu, wana nguvu zaidi ya Mungu?
-La.

9. Je, Mungu alifundishwa na mtu kuumba kila kitu?
-La.

10. Kwa nini hakuna aliyemfundisha Mungu?
-Kwa sababu hapo mwanzo, hakukuwa na yeyote ambaye angemfundisha Mungu.
-Pia, Mungu haitaji kufundishwa.

11. Je, kuna kipimo kwa hekima ya Mungu?
-La.

12. Je, kuna aliye na hekima zaidi ya Mungu?
-La.

-Hapo mwanzo, Mungu aliziumba mbingu na dunia.

-Wacha tusome jinsi dunia ilivyokuwa kabla ya Mungu kuumba vitu vyote.

Tusome Mwanzo 1:1-2a

> 1-Hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na Nchi
> 2-Nayo nchi ilikuwa ukiwa tena tupu

-Ulimwengu ulikuwaje kabla ya Mungu kuumba?

-Hapo mwanzo, hakukuwa na mwangaza.
-Hapo mwanzo, giza lilizingira dunia nzima.

-Je, ungependa kuwa na siku bila ya mwangaza wa jua?
-La.

-Je, ungependa kuwa na usiku bila ya mwangaza wa mwezi?
-La.

-Je, ingesikitisha kutokuwa na mwangaza wowote duniani?
-Ndiyo.

-Hungeweza kumuona mwenzako.
-Hungeweza kuona ili upande mimea yako.

-Hamngeweza kuona ili mjenge nyumba zenu.

-Hapo mwanzo hakukuwa na mwangaza.
-Hapo mwanzo hakukuwa na ardhi kavu.

-Mwanzo maji yalizingira dunia nzima.

Tusome Mwanzo 1:2b

2-Giza lilikuwa limefunika vilindi vya maji na Roho ya Mungu ilikuwa ikitanda juu ya maji.

-Hapo mwanzo maisha hayakuwa duniani.
-Lakini Mungu Roho Mtakatifu alikuwepo.



-Mungu Roho Mtakatifu alikuwa akingojea kuanza kazi yake ya kuumba kila kitu.

-Mnakumbuka ya kwamba kuna Mungu mmoja pekee lakini amegawanywa kwa nafsi tatu ambao ni Mungu mmoja?

-Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu kwa pamoja waliumba vitu vyote.

-Hapo mwanzo Mungu aliumba nini siku ya kwanza?

Tusome Mwanzo 1:3

3-Mungu akasema, “iwe nuru.” Ikawa nuru.

-Siku ya kwanza Mungu aliumba nuru.

-Mungu aliumbaje nuru siku ya kwanza?
-Mungu aliumba nuru kwa kunena.

-Je, kuna yeyote isipokuwa Mungu anayeweza kuumba nuru kwa kunena?
-La.

-Ufuatao ni mfano:

-Usiku mmoja uko kwenye kichaka bila nuru.

-Hakuna nuru kutoka kwa mwezi wala nyota.
-Kuna giza jingi na huwezi kuona chochote.

-Je, unaweza kunena, “Iwe nuru,” na ikawa nuru?
-La.

-Lakini Mungu kwa kunena tu, nuru ikaumbika.

-Mungu alijuaje kuumba nuru?

-Mungu anajua kila kitu.
-Hakuna chochote ambacho Mungu hakijui.

-Je, ilikuwa ni vigumu kwa Mungu kuumba nuru?
-La.
-Kwa nini?

-Kwa sababu Mungu ni mwenye nguvu.
-Kwa sababu hakuna chochote asichoweza kufanya Mungu.

-Mungu alifikiria nini kuhusu nuru aliyoumba?

Tusome Mwanzo 1:4a

4-Mungu akaiona nuru, kuwa ni njema.

-Mwanga ulioumbwa na Mungu ulikuwa mzuri.

-Hii ni kwa sababu Mungu hana makosa.
-Hii ni kwa sababu kila anachofanya Mungu nikikamilifu.

-Wanaume hujenga nyumba na wakati mwingine paa zinavuja.



-Wanawake wanafinyanga vyungu na wakati mwingine vinavunjika.

-Lakini Mungu aliumba kila kitu kikamilifu.
-Kwa nini?

-Kwa sababu Mungu ni mkamilifu.

-Baada ya kuumba nuru Mungu alifanya nini?

Tusome Mwanzo 1:4b-5

4-Kisha Mungu akautenga Nuru na giza.
5-Nuru akaiita “Mchana” na giza akaliita “Usiku.”
Ikawa jioni, ikawa asubuhi; siku ya kwanza.

-Mungu alipoumba nuru, hakuondoa giza lote kwa jumla.

-Mungu alitenga sehemu ya giza kuwa usiku.

-Kungekuwaje kama Mungu hangebakisha giza?
-Hatungeweza kulala.

-Mungu alibakisha sehemu ya giza ili tuweze kulala.

-Kila afanyachofanya Mungu ni kikamilifu.

-Siku ya pili Mungu aliumba nini?

Tusome Mwanzo 1:6-8

6-Mungu akasema, Na liwe anga katikati ya maji, likayatenge maji na maji.

7-Mungu akalifanya anga, akayatenga yale maji yaliyo juu ya anga na yale maji yaliyo chini ya anga; ikawa hivyo.

8-Mungu akaliita lile anga Mbingu. Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya pili.

-Siku ya pili, Mungu aliumba mbingu.

-Mungu aliumbaje mbingu siku ya pili?
-Mungu aliumba mbingu kwa kunena.

-Je, ilikuwa vigumu kwa Mungu kuumba mbingu?
-La.
-Kwa nini?

-Kwa sababu Mungu ni mwenye nguvu zote.
-Kwa sababu hakuna kinachomshinda Mungu.

-Mungu alitenganishaje maji yaliyozingira nchi?

-Mungu aliyaweka maji mengine kutoka kwa nchi juu ya mbingu.

-Mungu aliyaacha maji yaliyobaki juu ya nchi.

-Mungu aliumba nini siku ya tatu?

Tusome Mwanzo 1:9-10



9-Mungu akasema, "Maji yaliyo chini ya mbingu na yakusanyike mahali pamoja, nchi kavu itokee." Ikawa hivyo.

10-Mungu akapaita mahali pakavu "Nchi" na kusanyiko la maji akaliita "Bahari." Mungu akaona kuwa ni vyema.

-Siku ya tatu, Mungu aliumba nchi kavu.

-Nani aliyaagiza maji yakusanyike ili kuwe na nchi kavu?
-Mungu.

-Kwa nini Mungu anaweza kuaagiza maji kukusanyika mahali na yakamtii?

-Kwa sababu Mungu ndiye muumba wa maji.

-Je, kama mtu angeenda kwenye mto, ana uwezo kuamuru maji yakusanyike ili apite katikati?
-La.

-Mungu aliumba nini kingine siku ya tatu?

Tusome Mwanzo 1:11-13

11-Kisha Mungu akasema, "Nchi na ioteshe mimea. Mimea izaayo mbegu, na miti izaayo matunda yenye mbegu." Ikawa hivyo.

12-Basi, nchi ikaotesha mimea izaayo mbegu kwa jinsi yake, na miti izaayo matunda yenye mbegu kwa jinsi yake. Mungu akaona kuwa ni vyema.

13-Ikawa jioni, ikawa asubuhi; siku ya tatu.

-Siku ya tatu Mungu aliumba mimea na miti yote.

-Mungu aliumbaje mimea na miti yote?
-Mungu aliumba mimea na miti yote kwa kunena tu.

-Ilikuwa ni vigumu kwa Mungu kuumba mimea na miti?
-La.
-Kwa nini?

-Kwa sababu Mungu ni mwenye nguvu zote.
-Kwa sababu hakuna chochote asichoweza kufanya Mungu.

-Kuna aini ngapi za mimea na miti ambazo Mungu aliumba?
-Nyingi ambazo haziwezi kuhesabika.

-Kwa nini Mungu aliumba mimea na miti mingi?

-Je Mungu anahitaji mimea na miti ili aishi?
-La.

-Mungu aliumba mimea na miti yote ili isaidie nani?
-Mungu aliumba mimea na miti yote isaidie binadamu.

-Kwa nini Mungu aliumba mimea na miti yote?
-Kwa sababu Mungu anatupenda sana.

-Kama hakungekuwa na miti ingewezekana kujenga nyumba?
-La.



-Mungu alituumbia miti kwa sababu anatupenda.

-Kama hatungekuwa na mahindi, mngekula nini?
-Vichache.

-Mungu aliumba mahindi kwa sababu anatupenda.

-Mungu aliumba nini siku ya nne?

Tusome Mwanzo 1:16-19

16-Basi, Mungu akafanya mianga miwili mikubwa; ule mkubwa utawale mchana na ule mdogo utawale usiku; akafanya na nyota pia.
17-Mungu akaiweka mianga hiyo angani iiangazie dunia,
18-ipate kutawala mchana na usiku, na kuutenga mwanga na giza. Mungu akaona kuwa ni vyema.
19-Ikawa jioni, ikawa asubuhi; siku ya nne.

-Siku ya nne Mungu aliumba jua, mwezi na nyota.

-Mungu aliumbaje jua, mwezi na nyota?
-Mungu aliumba jua, mwezi na nyota kwa kunena tu.

-Kwa nini jua, mwezi na nyota hazianguki kutoka mbinguni?

-Kwa sababu Mungu aliziweka mbinguni.
-Kwa sababu kazi ya Mungu ni kamilifu.

-Mungu aliumba nini siku ya tano?

Tusome Mwanzo 1:20-21 & 23

20-Mungu akasema, “Maji na yatoe makundi ya viumbe hai na ndege waruke angani.”

21-Basi, Mungu akaumba wanyama wakubwa sana wa baharini na aina zote za viumbe vyote hai viendavyo na kujaa majini; akaumba na aina zote za ndege wote. Mungu akaona kuwa ni vyema.

23-Ikawa jioni, ikawa asubuhi; siku ya tano.

-Siku ya tano Mungu aliumba samaki na ndege wote.

-Mungu aliumbaje samaki na ndege wote?
-Mungu aliumba samaki na ndege wote kwa kunena tu.

-Ilikuwa ni vigumu kwa Mungu kuumba samaki na ndege?
-La.
-Kwa nini?

-Kwa sababu Mungu ni mwenye nguvu zote.
-Kwa sababu hakuna asichoweza kufanya Mungu.

-Mungu aliumba aina ngapi ya samaki na ndege?
-Nyingi ambayo haiwezi kuhesabiwa.

-Kwa nini Mungu aliumba samaki na ndege wote?

-Je, Mungu anahitaji samaki na ndege ili aishi?
-La.



-Mungu aliumba samaki na ndege wote kusaidia nani?
-Mungu aliumba samaki na ndege kusaidia binadamu.

-Kwa nini Mungu aliumba samaki na ndege wote?
-Kwa sababu Mungu anatupenda sana.

-Mungu alisema nini kuhusu vyote alivyoumba?
-Mungu alisema kuwa kila kitu ni kizuri.

-Kwa nini Mungu aliweza kuumba kila kitu kikamilifu?
-Kwa sababu Mungu ni mkamilifu.

-Kila alichoumba Mungu hapo mwanzo kilikuwa kikamilifu.

-Hapo mwanzo hapakukuwa na miiba.
-Hapo mwanzo hapakukuwa na magugu.
-Hapo mwanzo mahindi yote yalimea vizuri.

-Mungu aliumba kila kitu kikamilifu kwa sababu anatupenda sana.